

KINA CHA FIKIRA



**KAULIYA
WALIBORA**

**"Ilikuwa
furaha iliyoje
kutangamana
na nguli huyu
wa fani ya
ubunifu na
taaluma
ambaye
aliegemea
sana katika
falsafa"**

Tarehe 9 Januari 2020 ndiyo siku aliyotuacha mkono mwandishi nguli Euphrase Kezilahabi, tukio amba-lo limeuacha ulimwengu wa Kiswahili katika jitimai kubwa. Kwa sababu tayari zimehojiwa kumhusu kwenye vyombo kama vile Taifa leo, BBC and Radio Maisha, ni rahisi kuhisi kwamba hapani tena la kusema kumhusu mwandishi huyu maarufu. Ila bado ninao mshawasha kusema mengine zaidi. Wanaosema husema hakuna ziada mbaya. Tena yamkini baadhi ya wasomaji wangu hawakuwahi kusikia kauli zangu fupi kuhusu mwandishi mwenzangu katika vyombo hivi ya habari.


Mimi mwanzo nimekutana na Prof Kezilahabi katika vitabu vyake. Nime-kisoma mwanzoni kabisa nikiwa kida to cha kwanza kitabu chake cha awali *Rosta Mistika* kilichozaa kashesh. Nilivutiwa na ujumi wa usahihi wa kazi hiyo, alama ya utambulisho wa kazi zake zote. Kitabu chenyeh msuko sahili na lugha sahili kwa jicho la kizembe.

Ila ukichanganua vizuri unakumba na vito na lulu tele zilizofichama humo. Kwa kweli baadaye niliposoma vitabu vyake vingine kama vile *Dunia Uwanja wa Fujo, Kichwamaji, Kap-tula la Karl Marx*, na *Karibu Ndani* niligundua ugumu uliofichama ndani ya kile kinachoonekana kama usahili wa mtindo wake.

Utata na usahili unafikia kilele chake katika kazi zake za *Nagona na Mzingile* ambazo mpaka sasa bado hunitoa kijasho ninapozisoma. Wataalamu wa ndani na nje ya Afrika Mashariki wameandika makala za kila nui kuzilhusu kazi za Kezilahabi, mwandishi ambaye naye aliwahi kuandika kwa uketo kuhusu Shaaban bin Robert.

Miongoni mwa waandishi walibobeaa katika uhakiki wa kazi za Kezilahabi ni Prof Kyallo Wadi Warmitila na Dkt Ahmad Kipacha. Kwa kweli kama fasiri ya Nagona na Mzingile inakutatiza hao ndio watu wa kuwaomba wakusaidie kutanzua utata.

Ulimwengu wa Kiswahili umepigwa pufe na johari adimu Prof Kezilahabi



Nilipata fursa ya kukutana naye Kezilahabi mara kadha katika mabara matatu duniani. Niliwahi kukutana naye kwenye mji wa Madison Marekani alipoalikwa kutoa mhadhara katika Chuo Kikuu cha Wisconsin-Madison alikokuwa amepatia shahada yake ya uzanifu awali. Nilipata fursa nzuri ya kutangamana naye, kupiga soga naye na kula naye na kufaidi ucheshi wake wa kupindukia. Ilikuwa furaha iliyoje kutangamana na nguli huyu wa fani ya ubunifu na taaluma ambaye aliegemea sana katika falsafa!

Nilikuwa naye pia Ujerumani kwenye makongomano ya kila mwaka yanayoandaliiwa kwenye mji wa Bayreuth ambapo mihadhara yake ya kus-

isimua ilikuwa ikipokelewa kwa hamu na gharnu. Aidha nilikutana naye Afrika, kwenye Chuo Kikuu cha Botswana alikokuwa anafundisha kwa miaka mingi.

Sasa hatunaye tena, kaenda njia ya marahaba. Msiba huu si wa familia yake peke yake bali ni msiba wa jumuiya nzima ya wapenzi wa Kiswahili na fasih yake. Sisi "Waswahili" tulio-kumbana naye vitabuni na maishani tulimfahamu. Ndiyo maana tunamilii mwenzetu, tunaombeleza ingawa baadhi ya watu wanasema tunashere-hekeea maisha yake. Nje ya mawanda ya Kiswahili hata hivyo, hakujulikana Kezilahabi.

Nasema makiwa kwa msiba huu.